| JINA LA MTAHINIWA | |
|---|---|
| JINA LA SHULE YAKO | |
| SAHIHI YA MTAHINIWA | |

| NAMBARI YA MTAHINIWA | |
|---|---|
| NAMBARI YA SHULE | |
| TAREHE | |

# JUNIOR SCHOOL ASSESSMENT

# GREDI YA 9

JESMA 003

003-2025

Karatasi ya 1
Muda: Saa 1 dakika 40

## - KISWAHILI LUGHA -

### MAAGIZO KWA WATAHINIWA

1. Umepewa **kijitabu** hiki na **karatasi ya majibu.** Kijitabu hiki kina maswali **50.**
2. Jibu maswali **yote** kwenye **karatasi ya majibu** uliyopewa kujibia maswali na wala **sio** katika kijitabu hiki.

### JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU

3. Tumia penseli ya kawaida, aina ya HB.
4. Hakikisha kuwa **karatasi ya majibu** uliyopewa ina:
   **NAMBARI YAKO YA MTIHANI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**
   **JINA LA SOMO**
5. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.
6. Kwa kila swali, **1 - 50** umepewa majibu manne, A, B, C, D. Chagua **jibu sahihi.**
7. Kwenye karatasi ya majibu, onyesha jibu sahihi kwa **kuchora kistari** katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa jibu sahihi.

**Mfano:**
**Katika kijitabu cha maswali:**

25. Andika kinyume cha neno lililopigiwa mstari katika sentensi ifuatayo;
    Mpishi alikata mboga kwa kisu **kikali**.

A. Kibaya B. Kizuri C. Kizee D. Butu

Jibu sahihi ni **D.**

**Katika karatasi ya majibu,** palipo na visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba **25,** chora kistari ndani ya kisanduku chenye herufi **D.**

**25.** [A] [B] [C] [D]

8. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze **nje** ya kisanduku.

9. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku **kimoja tu,** kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kijitabu hiki cha maswali kina kurasa 8 zilizopigwa chapa. Hakikisha kuwa kurasa zote zipo na maswali yapo ipasavyo.**

GEUZA UKURASA


Tovuti: www.jesmapublishersltd.com Baruapepe: jesmapublishers@yahoo.com
*© Jesma Publishers & Educational Boosters Ltd. Tel: 0794677748/0701545759*
*WARNING: It is an offence to reproduce, copy or transmit whole or part of this paper on any social media platform. Any person contravening this is liable to criminal prosecution and civil claims for damages.*

***Soma kifungu hiki kisha ujibu swali la 1 hadi la 6.***

Komba hakuwa na marafiki. Wanyama wote mwituni walikuwa wakimkashifu kwamba alijiona kuwa na thamani kuliko wanyama wote duniani. Siku zote komba alijitenga na wenzake kwa kujificha katika vichaka ili asionekane.

Wanyama walikuwa wameizoea hali hiyo ya komba. Walimdhania kuwa wazimu na kuacha kushughulika naye. Walimwangalia kwa jicho la pembeni wakishangazwa na kile kilichomfanya kuwaepuka wenziwe. Kwanza, walimwona kama kijinyama kisicho na nguvu wala uzuri wowote. Kwao, komba alikuwa kinyangarika. Walichokosa kuelewa ni sababu ya yeye kuwa na tabia hiyo.

Ukweli ni kwamba komba alikuwa mnyama mwenye haya, jambo ambalo wanyama hawakulifahamu. Asingeweza kumwangalia mnyama yeyote machoni. Hakumudu kuzungumza na mnyama yeyote. Hata yeye mwenyewe, aliona tabia yake kuwa udhia mkubwa. Lakini, jivyo ni **jitihada haiondoi kudura**.

Baada ya kuona kuwa wanyama wenzake hawakumpenda, komba alijaribu kutafuta msaada. Wakati huu, ilikuwa ni vigumu sana kumsongea mnyama yeyote na kumweleza shida zake. Aliwazia kumweleza tumbili, lakini kila alipofika karibu na nyumba ya tumbili, alibadili nia na kurudi kwake. Alifikiri sana jinsi atakavyoanza kumwelezea tumbili shida zake, lakini hakuona namna.

Kwa sababu hii, komba alianza kuwa mnyama mwenye huzuni sana. Mawazo mengi yalimjaa kichwani nusura yamfanye kurukwa na akili. Hakuweza kutambua jinsi wanyama wenzake wanavyomdhania. Alijiona kuwa haini. Komba alilia kwa huzuni na upweke. Hakuweza kutambua kilichomfika. Mawazo yalizidi kumkodisha na kuwa mwembamba kama sindano. Aliimba nyimbo za huzuni na za kujikashifu mwenyewe.

Siku moja komba alipiga moyo konde. Komba aliamua kutenda lisilo budi. Aliwaendea wanyama wenzake kwa lengo la kuanzisha gumzo. Hata hivyo, hakuna mnyama aliyekuwa tayari kuzungumza naye. Kila mara alipojaribu kusogelea mnyama yeyote, alimkimbia kama aliyeugua ugonjwa wa ebola wasitake hata kumwona. Akasalia kuamini kuwa na maswali yasiyokuwa na majibu.

Siku moja, komba alijificha wakati wa usiku mahali ambapo asingeweza kuonekana na yeyote. Alinyemelea mnazi uliokuwa karibu, akaukwea mpaka kwenye kilele. Akaanza kunywa madafu. Kisha akapata tembo la mnazi, akanywa mpaka akalewa chakari. Komba mwenye haya aligeuka mlevi chakari.

Alifikiri pombe ingemwondolea upweke huo lakini haikumwondolea mawazo wala haya bali aliendelea kucheka sana. Hadi leo komba huwa na haya ile ile na kucheka zaidi hata usiku.

**1.** Kulingana na aya ya kwanza, ni kwa nini wanyama walimkashifu komba?
- A. Alikuwa na majidifu mengi
- B. Aliwatenga wanyama wengine
- C. Alikuwa mwenye haya kuliko wanyama wote
- D. Walimwona kama ana thamani kuliko wanyama wote

**2.** Methali **jitihada haiondoi kudura** inaweza kuwa na maana;
- A. Mungu si binadamu
- B. bidii huzidi uwezo wa Mungu
- C. kudura ni kubwa kuliko jitihada
- D. maamuzi ya Mungu hayawezi kubadilishwa

**3.** Komba alikusudia kumweleza nani shida zake?
- A. Nyani
- B. Tumbili
- C. Sokwe
- D. Nyumbu

4. Kulingana na kifungu hiki, ni kweli kusema;
   A. Komba alikuwa kinyangarika
   B. Komba aliwatenga wanyama wengine
   C. Komba alidhani wanyama wengine wana akili punguani
   D. Wanyama wenzake hawakuelewa kilichomfanya komba kuwa na hulka ile

5. Ni jambo lipi komba alipiga moyo konde na kuwaendea wanyama;
   A. kuanzisha mazungumzo ili wamwelewe zaidi
   B. kuambia wenzake kuwa ataanza kuanza kunywa pombe
   C. kuwa angetaka kupanda mti
   D. alijiona kuwa na huzuni na haya

6. Kulingana na kifungu hiki, kwa nini komba aliimba nyimbo za huzuni?
   A. Mawazo yalimdhoofisha zaidi
   B. Wanyama wenzake walimpongeza
   C. Kuuliza wanyama wenzake kwamba wamkaribishe
   D. Kuwaonyesha kuwa anapaswa kuheshimiwa

***<u>Soma kifungu hiki kisha ujibu swali la 7 hadi la 10.</u>***

Watoto wana wajibu wa kuhakikisha mshikamano katika familia zao. Aidha, wanastahili kuwaheshimu wazazi wao,wakubwa wao na watu wazima kila wakati na kuwasaidia wanapohitajika. Jukumu hili linapaswa kutekelezwa kutegemea maongezi na usaidizi wa wazazi.

Wazazi wanapowaongoza watoto wao wanastahili kuzingatia maoni yao. Maoni ya watoto hayafai kupuuziliwa mbali kama kwamba hayana maana yoyote. Watu wazima wanapaswa kuzingatia maoni ya watoto. Watoto wana jukumu la kutumia uwezo wao wa kimwili na kiakili kulihudumia taifa ili waweze kutimiza mahitaji ya kitaifa.

Serikali ni lazima kama ibada iwasaidie watoto katika kutekeleza jukumu hili. **Watoto wana jukumu la kutunza na kuimarisha umoja wa kijamii na taifa**. Wanapaswa kutunza na kuimarisha mila na desturi nzuri za jamii yao.

Hivyo basi ni sharti watoto wakubali na kujibidiisha kujifunza na kutokubali mila mbaya za jamii,na hawapaswi kutengwa kwa kutoa maoni ya kupinga mila hizo.

Jambo la kusikitisha hata hivyo ni kwamba ulinzi huo unaotolewa na makubaliano kuhusu haki za watoto hauwezi kutekelezwa na mahakama nchini Kenya. Hii ni kwa sababu kwa mujibu wa sheria za Kenya na mikataba ya kimataifa inayotiiwa sahihi na Kenya haiwi sheria hadi bunge lipitishe sheria hizo zitumike nchini Kenya.

7. Kulingana na aya ya kwanza;
   A. serikali ni sharti isaidie jamii
   B. taifa ni sharti lishughulikiwe na wachache
   C. watoto wana jukumu la kudumisha mshikamano wa jamii zao
   D. watoto wana jukumu la kudumisha mshikamano wa taifa

8. Ni jambo lipi ambalo halikutajwa kama wajibu wa watoto?
   A. Kuwatambua watu wazima kwa heshima
   B. Kuwapa heshima wakuu wao
   C. Kuwabeza wazazi wao na kuwadunisha
   D. Kuwaauni wazazi wao wanapowahitaji

9. Kulingana na kifungu hiki, maoni ya watoto hayafai kupuuzwa kwa sababu;
   A. ndio viongozi wa kesho hivyo basi wasubiri
   B. wanaweza kutumia maarifa yao kutunza taifa
   C. hawajakomaa kutoa maoni kamilifu ya kuifaa jamii
   D. wazazi wao wanapaswa kufikiria kwa niaba yao

10. Kauli **'watoto wana jukumu la kutunza na kuimarisha umoja wa kijamii na taifa'** imetumika katika kifungu hiki.Ni methali ipi isiyoambatana na kauli hii?
   A. Jifya moja haliinjiki chungu
   B. Kofi hazilii ila kwa viganja viwili
   C. Ukuni mmoja hauwaki mekoni
   D. Samaki mkunje angali mbichi

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 11 hadi la 15.***

Bibi huyo alikuwa mpole ilhali mumewe alikuwa simba pale chengoni pao. Bibi alikuwa mchwa kazini mwake. Alikuwa akirauka alfajiri na mapema ili kutayarisha staftahi ya watoto wake na ya simba wake. Aliwakama ng'ombe akawapa malisho na kung'oa nanga kuelekea kondeni.

Kwa kawaida mumewe aliamka baada ya jua kukausha umande. Baada ya kupata kiamshakinywa, hakuwa na jingine ila kuelekea madukani ambapo angelaza damu na wenzake waliokuwa na tabia hiyo. Hawakuwa na lolote la maana ila tu kupiga ngumzo hadi machwa. Baadaye walikuwa wakirejea nyumbani pao ambapo walipata kilalio huku wakikagua shughuli za wake wao za kutwa nzima.

Mbali na hayo yote, bibi huyo hakufa moyo. Aliendelea kuvumilia maudhui ya mumewe. Alikuwa na chembe ya matumaini kuwa mambo yangemwendea vyema. Alitarajia siku moja mumewe abadilishe mienendo yake kwani mui huwa mwema. Lakini tarajio ni jambo tofauti na uhalisi wa mambo. Mumewe alizidi kuwa katili.

<u>**Mambo yalizidi unga**</u> bwana mtu alipoanza kumpiga bibi yake bure bilashi. Maskini bibi mtu hakuwa na la kusema wala kufanya kwani mwenye nguvu mpishe na angurumapo simba mcheza ni nani?

Asubuhi moja, bibi huyo alipigwa sana na mumewe. Aliuma meno na kushika njia kuelekea kondeni. Mume naye alibarizi nje na kuota jua mwanana la asubuhi. Akiwa njiani kuelekea shambani, bibi yule alikutana na wanaume wawili. Walimsalimia kisha wakamweleza kuwa walikuwa wametoka nchi ya mbali. Lengo la kufika pale lilikuwa ni kumpata mganga stadi ambaye angemtibu mfalme wao.

Bibi mtu aliiona ile ikiwa nafasi nzuri ya kulipiza kisasi. Aliwaza na kuwazua kisha akawajibu wageni wale. "Hapa kariani tunaye mganga mmoja hodari sana. Yeye huyatibu maradhi ya kila nui. Hata hivyo ni nadra na adimu kama wali wa daku yeye kukiri kuwa ni mganga. Ninasikitika itabidi mmpige vikali ili akubali."

Watu wale walimwahidi mama yule kufanya juu chini kadri ya uwezo wao mradi wapate walichohitaji. Papo hapo, mama aliwaeleza wanaume wale njia ya kufuata hadi kwa mumewe. Walimpata maskini mwanamume yule akiota jua na walipomweleza walichotaka, mzee yule <u>**alikula yamini**</u> kuwa hakuwa na ujuzi wowote wala tajriba ya uganga. Walimchapa hadi akapoteza fahamu. Alipopata fahamu,alikubali shingo upande ili ayanusuru maisha yake alipoona kifo kinamkondolea macho.

Tayari malengo ya bibi yake ya kulipiza kisasi yalikuwa yametimia. Mume yule alimaizi kuwa si vyema kumdhulumu mwenzako au kumdhalilisha kutokana na udhaifu fulani . Anaweza kutumia njia mbadala na kukuadhibu kwa njia moja au nyingine.

Hata hivyo, yafaa watu waelewane kwa sababu la muhimu ni kuomba msamaha ili watu waishi kwa umoja, upendo na amani.

**11.** Kwa nini bibi alikuwa akiamka alfajiri na mapema? Ili

A. kutayarisha kisebeho cha familia yake

B. kuwakamua ng'ombe na kuenda kondeni

C. Ili kuwakama ng'ombe na kuenda sokoni

D. Ili kuonyesha mumewe kuwa yeye ni mtu wa bidii

**12.** Tangu mwanzo, bibi alikuwa na matarajio gani? Ya

A. mumewe kubadilisha tabia zake na kuwa mwema

B. kutangazia majirani kuwa mumewe ni mlaza damu

C. kulipiza kisasi kutokana na vile mumewe alimtesa

D. kuwatunza ng'ombe wake ili awe akipata maziwa tele

13. **Mambo yalizidi unga** ni kauli ambayo imetumika katika kifungu hiki. Unadhani ni mbinu gani ya lugha?

A. Methali

B. Nahau

C. Istiari

D. Tanakali ya sauti

14. Ni orodha ipi ya matukio ya mama iliyo sahihi kulingana na kifungu hiki?

A. Kiamshakinywa → kukama ng'ombe → kulisha ng'ombe → kuenda kondeni

B. Kiamshakinywa → kulisha ng'ombe → kuenda kondeni → kukama ng'ombe

C. Kiamshakinywa → kukama ng'ombe → kulisha ng'ombe → kuenda kondeni

D. Kuenda kondeni → kulisha ng'ombe → kukama ng'ombe → kiamshakinywa

15. Kwa mujibu wa kifungu hiki, ni kweli kusema;

A. mzee aliaga dunia mara tu alipopokea kipigo cha wanaume wawili

B. mama hakuenda kondeni siku alipokutana na waliompiga mzee

C. mzee alikuwa amefahamu kuwa mama alikuwa amempangia njama

D. mama hakumweleza mume wake kuwa ndiye alimpangia njama ya kupigwa

***Soma kifungu hiki kisha ujibu swali la 16 hadi la 20.***

Katika maisha ya binadamu hakuna jambo muhimu kama kuwa na afya bora. Afya bora inamwezesha mtu kufanya kazi na kujitimizia mahitaji yake. Pia mtu kama huyu huweza kushiriki kikamilifu katika shughuli mbalimbali za ujenzi wa taifa.

Je, ni kwa namna gani mtu anaweza kuwa na afya bora? Kwanza ni lazima ale vyakula vinavyo timiza mahitaji yote ya mwili. Kuna vyakula ambavyo huleta nguvu mwilini. Vyakula hivi ni kama vile mkate, wali, viazi na mihogo. Vyakula vya kuongeza nguvu vinajulikana kwa jina kabohaidreti au wanga.

Kuna vingine ambavyo hujenga mwili vinavyojulikana kama protini. Baadhi ya vyakula vya kujenga mwili ni nyama, maharage, maziwa, samaki na mayai. Pia kuna vile vinavyosaidia mwili kujikinga na maradhi kwa urahisi yaani vitamini. Hivi navyo ni vyakula kama mboga na matunda.

Maji ni muhimu sana. Sehemu kubwa ya mwili wa bindamu huchukuliwa na maji. Tuhakikishe kuwa maji tunayokunywa yamechemshwa sawa au yametiwa dawa ya kuua viini vinavyoweza kutudhuru. Tukinywa maji machafu au vyakula vichafu tunaweza kuugua maradhi ya tumbo.

Inatupasa vilevile kuiweka mili yetu katika hali ya usafi. Tunaweza kufanya hivyo kwa kuoga vizuri, kupiga meno yetu mswaki na kukata kucha zetu. Hali kadhalika ni sharti kama ibada tufue nguo zetu, tuzipige pasi, na tusafishe nyumba na malazi yetu. Kwa jumla ni lazima tuishi katika mazingira safi.

16. Ni mtu wa aina gani anayeweza kutumikia nchi vizuri? Mtu

A. aliye safi

B. anayefanya kazi

C. anayefanya mazoezi

D. mwenye afya bora

17. Vyakula kama vile nyama, maharage na maziwa vina faida katika mwili. Vyakula hivi huwa vimeorodheshwa katika kundi lipi la vyakula?

A. Protini B. Vitamini

C. Wanga D. Kabohaidreti

**18.** Kulingana na kifungu hiki,tunawezaje kuweka mili yetu safi kwa;

A. kuoga mtoni, kufua nguo na kula vizuri

B. kuosha nywele, kufua nguo na kukata kucha

C. kuoga,kupiga meno mswaki na kukata kucha

D. kuoga, kuvaa nguo vizuri na kukata kucha

**19.** Magonjwa matatu yanayotokana na maji machafu ni;

A. kuumwa na kichwa, kukohoa na mafua

B. ugonjwa wa malaria,ukimwi na saratani

C. ugonjwa wa upele,pepopunda na ukambi

D. ugonjwa wa homa ya matumbo, kipindupindu na kuhara

**20.** Mambo yapi mawili yanayopaswa kufanyiwa maji kabla ya kuyanywa?

A. kuchotwa na kuwekwa vizuri

B. kuchemshwa na kutiwa dawa

C. kuwekwa kwenye chupa na kufunikwa

D. kuwekwa kwenye friji kwa muda mrefu

***Soma kifungu hiki kisha ujibu swali la 21 hadi la 25.***

**Faraja** : Sabalkheri Katana! Naona una kipakatalishi tena. Ni lazima siku hizi umezama kweli kutafuta maarifa.

**Katana** : Aheri Faraja. Ni kweli! Nimekata kauli. Kama wasemavyo mtaka cha mvunguni sharti ainame. Kifaa hiki cha kidijitali ni kama mwalimu wangu anipendaye ambaye hachoki kunipa maarifa.

**Faraja** : Ajabu! Kwa kweli teknolojia imeleta darasa zima katika vidole vyetu. Kwa kufyatua herufi moja tu, tunapata maarifa ya busara ya wasomi wa hapo kale bila hata kutoka nyumbani na kuingia darasani kusoma na wengine.

**Katana** : Hapo umesema ukweli Faraja Nyanya yangu alikuwa kila akinikumbusha mara kuwa atangaye sana na jua hujua. Aidha mtoto ambaye hajawahi tembea kwingine hufikiri kuwa mama yake ndiye pekee hujua kupika. Hivi sasa, tunatembea bila kutoka kwenye viti vyetu.

**Faraja** : Katana, na usisahau smati bodi iliyoko darasani. Bodi hizo zimechukua nafasi ya mbao zilizokuwa zikitumia chokaa na kwa njia hiyo kurahisisha masomo darasani.

**Katana** : Ndio, halikadhalika, siku hizi badala ya kubeba matopa na matopa ya vitabu, tunabeba vifaa vya kidijitali na kuifanya kazi kuwa rahisi hivyo basi kuepukana na mzigo wa vitabu.

**Faraja** : Hata hivyo ni sharti tutumie teknolojia kwa njia nzuri. Kisu kikitumiwa vizuri, huwa cha manufaa makubwa na hutengeneza chakula kitamu, lakini kikiangukia mikono isiyojali husababisha madhara makubwa.

**Katana** : Nakubaliana nawe asilimia mia kwa mia. Ndiposa walimu na wazazi wanapaswa kutupa ushauri nasaha. Kuganda sana kwenye skrini huwa ni kama kuweka sukari nyingi kwenye kikombe cha chai. Wanasema ngoma ikipigwa sana hupasuka kiambo. Kilichotarajiwa kuwa kitamu hatimaye huwa chungu.

**Faraja** : Hayo yote ni ya kweli Katana: ikitumika kwa njia bora, teknolojia hutusaidia kung'aa kama nyota angani. Inaweza pia kusaidia wanafunzi kunawiri masomoni na kuendelea kusomea nyumbani bila matatizo yoyote.

**Katana** : Umesema ukweli. Elimu ni taa gizani hung'aa na teknolojia ndiyo hutunoa kila wakati. Tuitumie kuboresha maisha yetu ya usoni.

21. Katana analinganisha kipakatalishi chake na nini?
A. Mwalimu aliyechoka
B. Mwalimu mzuri
C. Mzazi mkali nyumbani
D. Mwanafunzi mashazari

22. Kulingana na mazungumzo haya, ni vipi teknolojia imeimarisha masomo?
A. Kubadilisha vitabu na nyimbo
B. Kufanya vitabu kuwa mzigo
C. Kuleta maarifa katika vidole vyetu
D. Kupuuza shule kuwa hazifai wakati wa teknolojia

23. Katana ametumia methali gani kueleza umuhimu wa masomo mtandaoni?
A. Elimu ni taa gizani hung'aa
B. Atangaye sana na jua hujua
C. Ngoma ikipigwa sana hupasuka
D. Asiyeskia la mkuu huvunjika guu

24. Unafikiri ni kwa nini Faraja alionya kuhusu kutumia wakati mwingi kwenye skrini?
A. Kwa sababu huifanya chai kuwa tamu
B. Kwa sababu inaweza kuwa na madhara
C. Kwa sababu hufanya teknolojia kupotea
D. Kwa sababu vitabu ni bora kuliko skrini

25. Ni funzo lipi wanafunzi wote wawili walijifunza?
A. Teknolojia hutumika badala ya walimu
B. Teknolojia ni hatari na inapaswa iepukwe
C. Teknolojia yafaa kutukiwa kwa busara kuleta manufaa
D. Shule hazipaswi kutumia skrini wakati huu wa teknolojia

***Kifungu kifuatacho kina nafasi 26 hadi 35. Umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kujaza nafasi***

Siku hizi uwanja wa mawasiliano __26__ sana. Tarakilishi ndiyo ala mojawapo __27__ sana __28__ mawasiliano. Njia __29__ hutumika zaidi ofisini. Aidha , ni kati ya matokeo ya maendeleo ya teknolojia maarufu kama teknohama __30__ dunia kuwa kama kijiji tu. Ujumbe __31__ uitwao arafa hutumwa kwa rununu. Teknolojia ina manufaa __32__ isipokuwa __33__. Mataifa __34__ na mikasa kama vile __35__ kwa kupashana habari.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 26. | A. utapanuka | B. yatapanuka | C. umepanuka | D. imepanuka |
| 27. | A. zatumika | B. inatumika | C. zinazotumika | D. inayotumika |
| 28. | A. katika | B. bali na | C. mbali na | D. ndani ya |
| 29. | A. hizo | B. hiyo | C. hilo | D. hayo |
| 30. | A. iliyowezesha | B. iliyoliwezesha | C. yaliyoiwezesha | D. yaliyoliwezesha |
| 31. | A. fupi | B. ndefu | C. mfupi | D. refu |
| 32. | A. mengi | B. nyingi | C. mingi | D. nyingine |
| 33. | A. kuimarisha | B. kuyaboresha | C. kuyakuza | D. kuyasambaratisha |
| 34. | A. hupigana kumbo | B. hupigana jeki | C. hupigana kifua | D. hupigana makofi |
| 35. | A. ugaidi | B. gharika | C. ufunzaji | D. utendakazi |

***Kutoka swali la 36 hadi la 50, chagua jibu sahihi.***

36. Kutokana na nomino **mchezaji** tunapata kitenzi
A. uchezaji B. cheza
C. mchezi D. mchezo

37. Chagua usemi wa taarifa wa sentensi hii;
Nitafanya bidii ili nikamilishe kazi yangu ya ziada, mwanafunzi aliahidi
A. Mwanafunzi aliahidi kuwa atafanya bidii akamilishe kazi ya ziada
B. Mwanafunzi alisema kwamba nitakamilisha kazi yangu ya ziada
C. Mwanafunzi aliahidi kuwa angefanya bidii akamilishe kazi ya ziada
D. Mwanafunzi aliahidi kuwa ataahidi kukamilisha kazi yake ya ziada

38. Kamilisha kauli hii:
Mngalikubali kuzungumza;
A. mngepatana B. mtapatana
C. mngalipatana D. mtazidi kupatana

39. Chagua sentensi yenye '**ki**' ya masharti.
A. Ukijitahidi utafaulu maishani
B. Mgeni alivalia kitamaduni
C. Kilikuwa kijitu kifupi sana
D. Walikuwa wakiningoja hapa tangu saa mbili

40. 'Ka' imetumikaje katika sentensi ifuatayo;
Alifika, akasubiri wakafika wakafanya mkutano wakaagana.
A. Kuonyesha wakati uliopita
B. Kuonyesha hali ya masharti
C. Kuonyesha hali ya mazoea
D. Kuonyesha mfuatano wa vitendo

41. Sahihisha sentensi hii;
Pale mlikohamia hamna mtandao mzuri
A. Pale mlipohamia hakuna mtandao mzuri
B. Kule mlikohamia hakuna mtandao mzuri
C. Mle mlimohamia hapana mtandao mzuri
D. Kule mlimohamia hakuna mtandao mzuri

42. Chagua sentensi yenye kihusishi sahihi cha '**a**' unganifu
A. Deni ya nyumba ililipwa jana
B. Pazia ya nyumba zimechafuka
C. Mbwa ya jirani yetu ni mkali sana
D. Gari la abiria huwa na mikanda ya usalama

43. Andika jibu la maamkuzi yafuatayo;
Waambaje?
A. Sina la kuamba B. Buheri wa afya
C. Sina utu D. Starehe

44. Wingi wa;
Seremala alifungua karakana yake jana.
A. Seremala walifungua karakana zao jana.
B. Maseremala walifungua karakana zao jana.
C. Maseremala walifungua makarakana yao jana.
D. Seremala walifungua makarakana yao jana.

45. Kiganja ni kwa mkono kama vile ______ ni kwa mguu
A. wayo B. nguyu
C. kisigino D. kisugudi

46. Ni sentensi ipi imetumia istiari?
A. Mwakio ni sungura siku hizi
B. Nyambura ni mpole kama njiwa
C. Muuguzi alisema mama huyo angejifungua salama
D. Moyo wake ulimwambia asikubali kuchukua hongo

47. Ikiwa juzi ilikuwa Jumatatu, Jumamosi itakuwa:
A. kesho B. mtondo
C. mtondogoo D. keshokutwa

48. Tumia '**amba**' ipasavyo katika sentensi:
Msitu unaohifadhiwa una wanyama
A. Msitu ambayo inahifadhiwa una wanyama
B. Msitu ambayo yanahifadhiwa ina wanyama
C. Msitu ambao unahifadhiwa una wanyama
D. Msitu ambao unao wanyama unahifadhiwa

49. Chagua kundi lenye vihisishi vya mshangao pekee.
A. Enhee ! Hewallah! Sadakta! Taibu!
B. Shabash! Masalaale! Oyee! Huree!
C. Lahaula! Salaale! Mama yangu! Mungu wangu!
D. Taib!, Naam! Abee! Taib! Enhee! Sadakta!

50. Chagua sentensi iliyo katika wakati uliopita hali timilifu:
A. Mjakazi alipika chakula kitamu
B. Mjakazi alikuwa amepika chakula kitamu
C. Mjakazi atakuwa amepika chakula kitamu
D. Mjakazi alikuwa akipika chakula kitamu